**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSIANA NA MSWADA WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA NA KUANZISHA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO.

**Mhe. Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako Tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake, ikiwemo kupitisha miswada mbali mbali. Mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na mambo yanayohusiana na hayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi maoni kuhusu Mswada niliokwishauainisha hapo juu.

**Mhe. Spika,** pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati serikali kupitia Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuwa na sheria madhubuti itakayoweza kulinda Maadili ya Viongozi lakini pia kuwapa imani wananchi juu ya utendaji wa viongozi wao.

**Mhe. Spika,** baada ya utangulizi huo Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora za kuwasilisha mswada huu muhimu ambao utasaidia

sana kupunguza ama kuondoa kabisa malalamiko ya wananchi juu ya viongozi wao lakini pia kuwafanya viongozi kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hatimaye wananchi kupata yale wanayoyatarajia kutoka kwa viongozi wao.

**Mhe. Spika,**dhana na maudhui ya Utawala Bora na Mswada wa Sheria hii ni kujenga jamii inayowajibika, yenye uwazi, inayoweka maslahi ya umma juu ya maslahi binafsi au ya mtu mmoja mmoja.

Aidha, sheria hii inalenga katika kuondosha upendeleo katika ajira, kupeana vyeo au nafasi yoyote ile ya madaraka kinyume na utaratibu uliowekwa kisheria.

**Mhe. Spika,** sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo waliujadili bila kuchoka ili kuhakikisha kwamba lengo la mswada huu linafikiwa na hatimaye nchi yetu inakuwa na sheria madhubuti na inayotekelezeka itakayolinda Maadili ya Viongozi wa Umma hapa Zanzibar.

Mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mhe. Spika,** naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Mjumbe

8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu.

**Mhe. Spika,**kutokana pia na maelekezo na ushauri wa Kamati ya Uongozi, kazi ya kuupitia mswada huu pia iwahusishe Wenyeviti wote wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi, hivyo kwa mnasaba huo pia, naomba kuwataja Wajumbe hao waalikwa kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin
2. Mhe. Ussi Jecha Simai
3. Mhe. Omar Ali Shehe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma
5. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, na
7. Mhe. Abdalla Juma Abdalla ( ambaye alikuwa Mjumbe mualikwa kwa ruhusa ya Mwenyekiti wa Kamati).

**Mhe. Spika,** naomba kuwatanabahisha Wajumbe kwamba marekebisho makubwa yamefanywa na Kamati yangu yamo kwenye orodha ya marekebisho ya Kamati waliyopatiwa, hii nisehemu ndogo tu ya marekebisho hayo. Hivyo, orodha ya marekebisho hayo pia ni sehemu ya hotuba hii.

**Mhe. Spika,** baada ya dibaji na tanbihi hiyo fupi naomba sasa nijilekeze kwenye marekebisho ya msingi yaliyofanywa na Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:

**Kifungu cha 29** kinachohusu "**Ripoti ya Mwaka ya Kazi za Tume**" kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno " **kwa mfumo wa kauli ya serikali**" baada ya neno "**kijacho"** mwishoni mwa kifungu.

Sababu ya marekekebisho haya ni kuepusha kufungua mjadala juu ya Ripoti ya mwaka ya kazi za Tume ndani ya Baraza na badala yake kutoa nafasi tu ya kuweza kuulizwa maswali Serikali juu ya Ripoti husika.

**Mhe. Spika,** kama maelezo ya Serikali kupitia Waziri Afisi ya Rais Ikulu na Utawala bora alivyowasilisha hapa Barazani wakati akitoa hotuba yake, madhumuni makubwa ya Serikali kuleta mswaada huu ni, kurejesha imani kwa wananchi kwa viongozi wao waliowachagua na wale waliopewa dhamana na Serikali kushika nafasi mbali mbali Serikalini, ili kujenga nidhamu, kuwa na maadili mema ya uongozi na dhamana walizopewa, kujenga uaminifu, kuondoa udokozi wa mali za umma, kuongeza uwajibikaji kwa umma, kulinda na kuhifadhi mali na dhamana walizopewa na wananchi na Serikali, ili kuongeza ufanisi na kuleta maendeleo kwa wananchi wote hapa Zanzibar.

**Mhe. Spika,** Serikali yetu katika kurejesha nidhamu katika utumishi wa Umma hapa Zanzibar, hivi karibuni ilileta Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi hapa Zanzibar, jambo ambalo lilikuwa linaleta ukakasi katika kutekeleza Sheria hiyo bila ya kuwepo kwa Sheria hii ya Maadili ya Viongozi wa umma, kwa hiyo kuletwa kwa Sheria hii, kutaipa nguvu Tume ya kupambana na Rushwa na kuhujumu Uchumi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

**Mhe. Spika,** kama jadueli la pili la Sheria hii ya maadili ya viongozi, Sheria inavyojieleza kuwa Mswada huu, unawahusu wakubwa na vigogo wa nchi, kwa hiyo utekelezaji wa Sheria hii unakuwa mgumu sana hasa kwa kuzingatia, nguvu na sauti waliyokuwa nayo katika nchi lakini pia uwezo wa kifedha walio nao, sasa tujiulize hii Tume itakayoundwa ya Maadili ni kweli itaweza kutenda haki katika kutekeleza kwa uadilifu katika kutoa haki na kusimamia majukumu yao bila ya kuingiliwa katika maamuzi yao? Lakini isitoshe, je, tujiulize ni kweli Tume hii itaweza kuibua mizengwe iliyofanywa na inayofanywa na viongozi waliopo madarakani na wale waliostaafu ambao hadi leo wanashikilia mali za umma na haki za wananchi wengine wanyonge? Sasa Kwa maoni yangu Tume hii imepewa mtihani mkubwa na sijui kama kweli wataweza kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu.

**Mhe. Spika,** kwa nini nikasema hivyo; Mhe Spika, wananchi wengi ambao ni wadau wakubwa katika Sheria hii hivi sasa wanaisubiri kwa hamu kubwa Sheria hii ili kuwaburuza wakubwa na vigogo kwenye Tume ya Maadili ili kudai mali zao walizozichukua kwa nguvu na kwa kutumia mamlaka waliyopewa na wananchi, lakini wengine walitumia nyadhifa zao kwa kuwanyang'anya mali zao na kuwapa aidha marafiki zao au watoto wao, kwa hiyo kwa Sheria hii vigogo hao wajiandae kuburuzwa kwenye Tume ili kuweza kujibu mashtaka yatakayopelekwa na wananchi dhidi yao, na pia tutaangalia ikiwa Tume itaweza kutumia mamlaka waliyopewa na Sheria hii kuweza kutoa ushauri kwa mamlaka husika kuweza kurejeshewa wanyonge haki zao pia kurejeshwa kwa mali za umma zinazomilikiwa na aidha viongozi au waliokuwa viongozi wakati walipokuwa madarakani.

**Mhe. Spika,** kwa kweli Serikali katika Sheria zote ilizoleta hapa Barazani, hii ndio Sheria ya mwanzo ngumu katika utekelezaji wake, kwani Mhe. Rais, atakuwa na mtihani mkubwa wa kutoa maamuzi magumu kwa wale wateuzi wake aliowapa dhamana ambapo wengine ni wapambe wake,marafiki zake, ndugu zake,jamaa zake na wakati mwengine hata yeye mwenyewe, kwani Sheria hii inawagusa wakubwa na vigogo watupu.

**Mhe. Spika,** Sheria kama hii ndiyo iliyomfanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kufanya mabadiliko makubwa kwenye Baraza lake la Mawaziri kwa zaidi ya mara tano katika kipindi chake cha uongozi akiwa Rais na mkuu wa nchi, na mfano mzuri ni matukio yaliyotokezea hivi karibuni katika kadhia ya fedha za akaunti ya ***(ESCROW)*** ambapo karibu mawaziri wawili na baadhi ya watendaji wa Serikali kuwajibishwa kupitia Sheria ya maadili ya viongozi kwa ushauri na mapendekezo ya Tume ya Maadili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Spika,** ndiyo maana tukasema hii ndio Sheria ngumu ya mwanzo katika utekelezaji wake, kwa hiyo kamati yangu inatoa wito kwa wale wote walioko karibu na familia ya Mhe Rais, mawaziri, majaji, Wawakilishi, na viongozi wengine waliotajwa kwenye Mswada huu na wale wote waliopewa dhamana aidha Serikalini

au kwa wananchi kujirekebisha makosa yao, na kama wako waliochukua mali za watu wazirejeshe kabla ya Mhe. Rais kuitia saini Sheria hii, vinginevyo Sheria hii itakuja kuwaumbua.

**Mhe. Spika,** tunaiomba sana Serikali yetu hasa Mhe. Rais, asiwafumbie macho wale wote watakaopelekwa kwake ambao waliogundulika wamevunja maadili ya uongozi kwa kuwachukulia hatua za kisheria kwa haraka ili kujenga imani kwa wananchi wetu, kwani hivi sasa kupitia ripoti mbali mbali aidha za Kamati teule zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi, na kutolewa ripoti hapa Barazani lakini utekelezaji wake umekuwa ukisuasua, pengine labda kwa udhaifu wa kisheria, lakini kupitia Sheria hii nadhani tutakuwa tumekupa nguvu kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale wote waliohusika.

**Mhe. Spika,** lakini pia bado kuna viongozi ambao bado wako madarakani ambao wamesababisha wananchi kukosa haki zao kwa kuwapa watu wengine aidha kwa kuwapa jamaa zao au rafiki zao au kuzichukua wao wenyewe, kwa hiyo pia kupitia mswada huu,sasa ni wakati wa kujisafisha kwa viongozi wote wa Umma hapa Zanzibar.

**Mhe. Spika,** katika mswada huu katika **kifungu cha 15** kinachoelezea viongozi kutangaza mali zao wao wenyewe na familia zao kabla ya kushika madaraka na kila baada ya mwaka mmoja na pia wakati anapoondoka madarakani ili kumfanya kiongozi wa Umma aaminiwe na kukubalika kwenye jamii.

**Mhe. Spika,** pia mswada umeelezea kiongozi kueleza ukweli mtupu katika kutangaza mali zao na ikitokea kudanganya litakuwa ni kosa na hatua za kinidhamu na kisheria zitachukua mkondo wake. Sasa kwa kifungu hiki tutaangalia ukweli wa viongozi katika kutangaza mali hizo, kwani kuna baadhi ya watu wenye dhamana wanamiliki mali ambazo hata ukifanya tathmini ya kipato chao, basi hawawezi kumiliki mali hizo, sasa suala linakujaje?

Tume itachukua hatua gani kwa wale watakaogundulika wamemiliki mali kinyume na uwezo wao kisheria? Kwa hiyo, wananchi wanaisubiri kwa hamu Tume hii jinsi itakavyoweza kuibua mambo kama hayo.

**Mhe. Spika,** pia Mswada huu umeelezea kiongozi au mtumishi awe muaminifu katika dhamana aliyopewa na wananchi au Serikali, lakini suala hili limekuwa ni sugu Serikalini kwani kwa nyakati tofauti tumesikia watu kuiba mali za umma zikiwemo nyaraka za Serikali, pesa taslim na hata baadhi ya samani za maofisini, lakini kama hiyo haitoshi kumekuwa na kadhia kubwa kubwa wa uvujaji wa mapato ikiwemo kwa malipo yanayolipwa au yaliyolipwa kwa wafanyakazi hewa ambapo Baraza lako Tukufu limemtaka Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kulifanyia uchunguzi suala hilo lakini cha kushangaza na kusikitisha hadi leo hatujaletewa ripoti hapa Barazani.

Kwa hiyo Mhe. Spika, kupitia Sheria hiyo tunamtaka Mdhibiti Mkuu kutuletea ripoti hiyo ya uchunguzi ili tuweze kuiagiza Serikali kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika na upotevu wa pesa hizo na wazirejeshe Serikalini. Kwani huo ni ukiukwaji mkubwa wa maadili ya viongozi wa Umma na Utumishi wa Umma.

**Mhe. Spika,** mimi naamini baada ya kupitishwa Sheria hii kuna baadhi ya viongozi na hata watendaji wataamua wao wenyewe kusamehe nyadhifa zao ili Sheria hii isiwakumbe, kwani itakuja kuwaumbua. Lakini pia waliobaki wataongeza bidii katika utendaji wao wa kazi kama **kifungu cha (16)** cha jadweli la Mswada huu kinavyoelezea.

**Mhe. Spika,** pia katika Sheria hii **kifungu cha 17** kimeelezea kuhusu kiongozi kuepuka kuweka maslahi binafsi katika utumishi wa Umma.

**Mhe. Spika,** bila kificho tatizo hili ni kubwa kwenye Serikali yetu, kwani kuna watendaji na viongozi ambao hutumia nyadhifa zao kwa kutumia mali za Umma kwa kujizalishia na kujilimbikizia mali wao binafsi, na mifano imo kwenye ripoti za kamati Teule za Baraza, na

wengine hutumia taarifa na mipango iliyomo kwenye wizara zao na kujiandaa aidha kujipatia ***"Tender"*** au kujipatia biashara kupitia mipango ya Serikalini, suala hili ni kubwa na ni ukiukaji mkubwa wa maadili, lakini pia suala la maslahi binafsi linasababisha hata baadhi ya miradi ya Serikali kuchelewa na pia kuwa haina viwango vya ubora, kwani kwanza wakubwa huchagua kampuni za marafiki zao na kuwapa kazi ambazo aidha hawana uwezo nazo au kuchukua rushwa ili kuweza kuwapatia ***"Tender"*** , na pia wakati mwengine pia viongozi huamua kwa makusudi, kulazimisha kukiuka baadhi ya maamuzi ya ***"Tender board"*** katika kutoa ***"Tender"*** ili yapewe Makampuni yao au ya jamaa zao ili na wao waje kufaidika na miradi hiyo, na mifano hiyo ipo hapa Zanzibar.

**Mhe. Spika,** lakini sisi kama Wajumbe tutakuja kuitumia Sheria hiyo kuja kupinga Kampuni hizo hapa Barazani ili kazi hizo wapewe zile Kampuni zilizoshinda kisheria, kwani tumechoka na miradi mibovu na miradi isiyokamailika kwa muda unaopangwa kutokana na rushwa na tamaa za watu wachache kwa faida zao.

**Mhe. Spika,** katika sheria hii pia limeelezewa kuwa kiongozi hatapokea zawadi akiwa katika utumishi wa umma isipokuwa zawadi hiyo itakuwa ni mali ya Umma  na atatakiwa aiwasilishe Serikalini.

**Mhe. Spika,** suala hili ni geni kwetu kwani tumezoea kuona na kusikia viongozi wetu kupewa zawadi mbali mbali ndani na nje,na wakati mwengine zawadi hizo haziletwi Serikalini lakini viongozi huzitumia wao wenyewe binafsi kwa kujinufaisha wao wenyewe, wakati mwengine wale wanaotoa zawadi hutoa kwa ajili ya kuwashawishi viongozi hao aidha kuja kufaidika na miradi au biashara zao, kwa hiyo tunatoa tahadhari kwa viongozi wote aidha wakubwa au wadogo kujiepusha na kupokea zawadi ambazo zitawasababisha kutoa upendeleo kwa watu hao, kwa hiyo kwa hivi sasa tunatakiwa tuwe makini katika kupokea zawadi hizo.

**Mhe. Spika,** pia katika Mswada huu kumetajwa suala la kuepuka kutoa upendeleo katika masuala mbali mbali ikiwemo suala la ajira.

**Mhe. Spika,** eneo hili ni kubwa na tunatakiwa kuchukua tahadhari kubwa kwani wakati mwengine wakubwa hutoa "vi-*memo'* kwa taasisi zinazotoa ajira ili watu au jamaa zao waweze kupatiwa ajira hata kama hawana sifa za kuweza kuajiriwa katika sehemu hizo, ndio maana tukasema hii ni miongoni mwa Sheria ngumu kuitekeleza hapa nchini, kwani kutokutii maagizo ya wakubwa hupelekea kuhatarisha ajira ya hao wanaopelekewa "vi-*memo*" hivyo.

Kwa hiyo, kwa kuwa ***Sheria ni msumeno,*** basi tujiandae na changamoto za sheria hii, kwani tatizo la Zanzibar ujomba tumeuweka mbele kuliko sifa na uwezo wa wanaopewa dhamana katika kazi, kwani wakati mwengine bila ya kificho kuna watu hupewa dhamana kubwa Serikalini wakati hawana uwezo wa kazi hizo na kupelekea kuikosesha Serikali huduma bora na kuchelewesha kasi ya maendeleo katika taasisi husika.

**Mhe. Spika,** mambo haya wananchi hawana uwezo nayo kwani yako katika mamlaka za uteuzi jambo ambalo linaidharaulisha Serikali kwa jamii, na wakati mwengine wale wanaopewa dhamana hizo huzitumia vibaya kwani wanajua kuwa wanalindwa na wakubwa waliowapeleka katika nyadhifa hizo kupitia migongo yao.

**Mhe. Spika,** katika mswada huu pia umeelezea matumizi mabaya ya madaraka, matumizi mabaya ya mali za umma ikiwemo matumizi ya magari mengi ya Serikali, lakini pia nyumba za Serikali, kwani kuna magari ya Serikali baada ya saa za kazi utawakuta watu wakiyatumia kwa shughuli zao binafsi, bila hata ya kibali cha Serikali, lakini pia kuna baadhi ya viongozi au waliokuwa viongozi hadi leo wanatumia nyumba za Serikali kinyume cha Sheria na Serikali imekaa kimya hakuna hatua zozote za kisheria.

**Mhe. Spika,** pia katika nyumba hizo baadhi yao wamefikia hatua za kuwarithisha jamaa au watoto wao, sasa hebu tujiulize, je, ikiwa kila kiongozi au mtumishi anayepewa kutumia nyumba ya Serikali kama hataki kuirudisha, je, nyumba hizo zitabaki? Au kuna Sheria gani ya kiongozi kugaiwa nyumba ya Serikali? Ndio maana pale mwanzo nikasema Sheria hii itakuwa ni ngumu kutekelezeka hasa kwa muhali ambao tumezoea kuchukuliana, lakini kwa kuwa ***Sheria ni msumeno,*** basi hatuna budi sote kwa pamoja tushirikiane katika kuitekeleza, hayo ndio maadili ya kila aliyekubali kuwa kiongozi wa Umma

**Mhe. Spika,** katika kifungu namba (2) cha Jadweli la Mswada huu umeelekeza viongozi kuheshimu Sheria na Utawala Bora na kuheshimu wananchi wote kwa ujumla, pia kuheshimu taratibu za kubadilishana madaraka katika chaguzi mbali mbali, kuheshimu uhuru wa Mahkama, kuwa na Serikali sikivu, Umoja wa Kitaifa.

**Mhe. Spika,** pamoja na kuheshimu uhuru wa Mahkama, lakini pia na Mahkama zenyewe kuwa waadilifu katika kutoa hukumu ili kulinda maadili ya Mahkama pamoja na Mahakimu wenyewe kujiepusha na kuvunja Sheria na kutoa maamuzi yasiyo ya haki hasa kutokana na nguvu ya Sheria, kwani tumeshuhudia kuwa kesi nyingi hasa za ubakaji na madawa ya kulevya zimekuwa hazipati hukumu ambazo wananchi wengi wamekuwa wakizitarajia, jambo ambalo huwafanya wananchi kukosa imani na vyombo vyetu vya kutoa haki.

**Mhe. Spika, lakini pia katika kif (7)cha jadweli la kwanza la Mswada huu kinaelezea kuwa "Serikali itakuwa na jukumu la msingi kuheshimu na kutekeleza maazimio ya vyombo vya kutunga Sheria yaani "BARAZA LA WAWAKILISHI**".

Kwa kifungu hiki sasa sisi tukiwa Wajumbe wa Baraza hili tutakuwa na haki ya kuidai Serikali utekelezaji wa maamuzi halali ya Baraza lako hili ikiwemo Kamati Teule za Baraza.

**Mhe. Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kuwashukuru Wajumbe wangu wa Kamati kwa kuweza kunipa mashirikiano muda wote hadi kuweza kukamilisha ripoti hii ya Kamati yako.

**Mhe. Spika,** aidha napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa na wa hali ya juu, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

............................

Hamza Hassan Juma.

Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
Baraza la Wawakilishi,
**ZANZIBAR.**